# HALMASHAURI YA WILAYA YA SHINYANGA

**Namba za Simu**
Mkuu wa Shule 0784168105
**M/Mkuu wa Shule 0652854925**

**Namba Mtaaluma 0695148655**

**Shule ya Sekondari Samuye**
**S.L.P 1023**
**SHINYANGA**

**07-05-2026**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi.**
**……………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**…………………………………………….**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI** SAMUYE **HALMASHAURI YA SHINYANGA MKOA WA SHINYANGA**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2026/2027 na atasoma tahasusi ya ………….

Samuye Sekondari iko katika kata ya Usanda,Tarafa ya Samuye,Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga,Mkoa wa Shinyanga.Ipo kando ya barabara kuu ya Shinyanga -Tinde,umbali wa 25KM kutoka Shinyanga mjini na 10 KM kutoka tinde mzani,usafiri kutoka Shinyanga mjini kuja shuleni ni wa uhakika na unapatikana wakati wote kwa gharama ya Tshs.2,000/=. Kwa wanaotoka nje ya Mkoa na kupanda mabasi utalazimika kushukia kituo cha Usanda ambayo iko takribani 1KM.kuja shuleni

**Muhula wa Masomo utaanza kwa tarehe itakayotangazwa na Ofisi ya Waziri Mkuu**

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**2.1 SARE YA SHULE (DARASANI)**

**A. WAVULANA**

(i) Njoo na suruali mbili (2),moja rangi ya khaki na nyingine kijani ya kibichi (kreta namba moja) suruali iwe na marinda mawili kila upande mbele na pia iwe imekunjwa chini (turn up) na yenye upana usiopungua inchi 16" chini, suruali za chupa hazikubaliki (**Rejea kiambatanisho C**).

(ii) Soksi nyeupe jozi mbili (2) fupi za kati
(iii) Viatu vya ngozi vyeusi vya kufunika na siyo buti wala gharofa (High Heeled Shoes) vya kufunga kwa gidamu (**Kamba**)
(iv) Mashati meupe (2) mikono mirefu yanayotosha kuchomekea.
(v) Sweta rangi ya kijani kibichi
(vi) Tai mbili(2) moja kijani kibichi na nyingine khaki

## 2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

(i) Madaftari 20 QUIRE 4
(ii) Rimu mbili (2) za karatasi nyeupe (A4) aina ya DOUBLE A (kwa mwaka)
(iii) Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (*Orodha imeambatanishwa katika kiambatanisho D )*
(v) Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma Biology (CBG)
(vi) Boksi moja la examination gloves kwa wanafunzi wote wanaosoma Biology kwa ajili ya dissection
(vii) Scientific Calculator kwa tahasusi za HGK na CBG
(viii) Ndoo moja (1) ya lita 20, mfagio mgumu mmoja na laini mmoja kwa kila mwanafunzi.
(ix) Jembe na mpini wake
(x) Squezer moja
(xi) Lita tano (5) ya dawa ya kusafishia vyoo kwa kila mwanafunzi

## 2.3 Michango mbalimbali Shule za Bweni

| **Na** | **Aina ya Mchango** | **Kiasi** |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

MICHANGO ILIPWE BENKI YA NMB: A/C NA. **30706600092**
JINA LA AKAUNTI YA MICHANGO: **SAMUYE SECONDARY *SCHOOL***

## 3 Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

(i) Heshima kwa viongozi,walimu, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
(ii) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
(iii) Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
(iv) Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
(v) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani ya shule na nje mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
(vi) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
(vii) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
(viii) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
(ix) Kutunza mali za shule;
(x) Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
(xi) Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

**Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

**Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

**Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule.**

### 3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:

(i) Wizi;
(ii) Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
(iii) Kugoma na kuhamasisha mgomo;
(iv) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;

(v) Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
(vi) Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
(vii) Kufuga ndevu;
(viii) Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
(ix) Uvutaji wa sigara;
(x) Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
(xi) Kupata ujauzito au kutoa mimba;
(xii) Kusababisha mimba;
(xiii) Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
(xiv) Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
(xv) Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
(xvi) Kudharau Bendera ya Taifa;
(xvii) Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
(xviii) Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**3.3 Viambatisho na Fomu Muhimu**

(i) Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali (**angalia kiambatanisho B)**

(ii) Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za Simu.

**3.4** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**.......................................................**
**JOHN ALBIN RODGER**

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO:**

**Mkuu wa shule 0784168105 / 0626790669**
**Makamu Mkuu wa Shule 0786989843**
**Mwandamizi Taaluma 0695148655**

# KIAMBATANISHO A

## MAHITAJI BINAFSI YA MWANAFUNZI

| NA | MAHITAJI |
|---|---|
| 1 | Godoro la sponji futi $3 \times 6$ |
| 2 | Blanketi kwa ajili ya baridi |
| 3 | Sanduku la chuma |
| 4 | Ndoo moja kwa ajili ya usafi binafsi |
| 5 | Mashuka manne (4), mashuka mawili ya rangi ya pinki na mawili light blue |
| 6 | Taulo, chupi au boxer za kutosha |
| 7 | Sabuni za kutosha |
| 8 | Mafuta ya kupaka |
| 9 | Lesso |
| 10 | Ndala / sendo / open shoes |
| 11 | Kiwi na brashi |
| 12 | Mswaki na dawa ya meno |
| 13 | Kitana |
| 14 | Kikombe cha uji / chai cha nusu lita |
| 15 | Kijiko |
| 16 | Kontena / lunch box kwa ajili ya chakula |
| 17 | Chandarua cha mstatili na si duara (ring) rangi ya light blue |
| 18 | Daftari kubwa (Counter Books quire 4) na kalamu za kutosha |
| 19 | |
| 20 | Suruali mbili (2) za kushindia rangi nyeusi zenye maridha mawili mbele, iwe na turn up na yenye upana usiopungua inchi 16", suruali chupa hazikubaliki (Rejea kiambatanisho A) |
| 21 | Tochi / kurunzi (Isiwe ya kuchaji kwa umeme) |
| 22 | Track suit pea moja (Rangi nyeusi) |
| 23 | |
| 24 | **VIFAA VYA MICHEZO**<br>- Soksi jozi mbili rangi nyekundu kwa ajili ya michezo.<br>- Viatu vya michezo<br>- Jersey ya Real Madrid (nyeupe) kwa michepuo ya sanaa na Jersey ya Bacelona (michirizi ya damu ya mzee na blue) kwa michepuo ya sayansi. |
| 25 | Tshirt za shule (darasani & kushindia) zinapatikana shuleni |
| 26 | Raba za kushindia rangi nyeupe kwa kila mwanafunzi<br>, |

**Tanbihi**

1. Mwanafunzi aje na Bank Pay in Slip moja (michango) ambayo ina jina la mwekaji ambalo ni jina la mwanafunzi husika
2. Mwanafunzi asije na nguo za nyumbani na simu haziruhusiwi kabisa
3. Mahitaji ya vitu vidogo vidogo yatapatikana ( yanauzwa) kwenye duka la shule
4. Fika mapema shuleni ( kabla ya saa 11:00 jioni) ili uweze kupokelewa na kupewa huduma mara ufikapo
5. Mwanafunzi anatakiwa kuvaa truck suit anaporipoti shuleni na si vinginevyo
6. Mwanafunzi ahakikishe amepima afya yake na kujaziwa fomu iliyoambatanishwa na maelezo haya kwenye hospitali / kituo cha afya cha serikali na siyo binafsi
7. Ni vyema wanafunzi mwenye **Bima za Afya NHIF** na zingine zinazokubalika waje nazo shuleni kwa ambao hawana bima za **NHIF** na wanazihitaji zinapatikana kwa 50,400/= tu kwa mwaka.

**KIAMBATANISHO B**

**SHINYANGA DISTRICT COUNCIL**

**SAMUYE SECONDARY SCHOOL**
**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

**PART A** Date
To the Medical Officer From ________________

__________________

__________________
Name of student in full_____________________________ please examine the above as to his / her physical and mental fitness for a full time study (two years course)

The examination should include:-

(i) (a) Eye – sight (b)Hearing (c) Speech (d) Limbs (e)Chest (f) Veneral Diseases (g) Epilepsy (h) Leprosy

(ii) Cirrhosis
(iii) Other diseases
(iv) Pregnancy (For ladies)

**PART B (To be completed by Government Medical Officer)**

I have examined the above named person and consider that he / she is physically and mentally

**FIT / UNFIT** for a full time of four years study / course.

(i) (a) Eye – sight_________________
(b) Hearing ___________________
(c) Speech____________________
(d) Chest_____________________
(e) Veneral Diseases____________
(f) Epilepsy___________________
(g) Neurosis___________________
(ii) (a) Neurosis_________________
(b) Cirrhosis_________________
(iii) Other serious diseases_________
(iv) Pregnancy __________________

**PART C**

Doctor's General
Remarks_______________________________________________________________
Signature:____________ Designation ________________Station__________________

# KIAMBATANISHO C (SARE)

<table>
<tr>
<td>
</td>
<td>
</td>
</tr>
<tr>
<td>KHAKI</td>
<td>KIJANI</td>
</tr>
</table>

*KIAMBATANISHO D*

## ORODHA YA VITABU KWA KILA SOMO

1. **HISTORIA**

Saleh Yassin (2010), Essentials in Advanced Level History One & History Two
Zisti Kamili (2010) History Advanced Level History One & History Two
Shibitali C.K ( 2012) Contemporary historical Events, Advanced Level History Two & History One

2. **JIOGRAFIA**

Monk House (1990) The principle of Physical geography
David Waugh (2009) practical Geography
David Waugh (2009) Integrated Approach Physical
Geography Zist Kamili (2010) Physical Geography Alive for
Advanced level Zist Kamili (2010) Human and Economic
Geography
Mtegetwa (20010) Practical Geography
Msabila D.T (2020 Practical Geography for Advanced
Level Msabila D.T. (2010) Human and Economic
Geography Pritchard John (2000) Practical Geography for
East Africa Pritchard John (2000) Economic Geography
for East Africa

3. **ENGLISH LANGUAGE AND LITERATURE IN ENGLISH**

Advanced Level Literature (Nyambari Nyangwine (2012)
Nicholous Asheli, Practical Approach, Literature (2012)
Betrayal in the City , Francis Imbuga
Selected Poems – TIE
An enemy of the people – Henrik Ibsen
A hand out for Advance, Paschal Salaw, need Level English
One I will Marry when I want – Ngugi wa Thiong’o
A man of the People – Chinua Achebe
The Beautyful Ones Are Not Yet Born – A.
Armah A season by Waiting – David Omowale
Advanced Level Literature – Nicholous Asheli
The Wonderful Surgeon and Other Poems by Charles Mloka

4. **BAIOLOJIA**

Taylor, D.J et al (2009) Biological science one & two 3rd Ed, Cambridge university Press, Edinburgh
Toole, G and Toole, S (1999) Understanding Biology for advances,
level Plants and animals biology vol I & II
Chand, S, Verna P.S and Pandey (2010) Biology for class
IX Botany for degree students by Dutta
Clegg, C.J and Mackean, D.G (1994): Advanced Biology, Principles and applications John Murray publishers LTD

5. **KEMIA**

TIE (2019, Organic chemistry for A-level Secondary Schools
TIE (2019), Inorganic Chemistry for A-Level Secondary Schools form five & six

TIE ( 2019), Physical Chemistry for A – Level Secondary Schools form five & six

TIE (2019) General Chemistry for A-Level Secondary School form five & six

Ramsden, E.N (2000). Advanced level chemistry (3rd ed). Cheltenham: Nelson Thrones publishers Ltd

**6. FIZIKIA**

Chand for class Xi and Xii

Tom Duncan

Rodger

Muncaster

Nelcon

Recipicious

Kiiza

**7. ADVANCED MATHEMATICS**

Sillen S.I (2014) Advanced Mathematics for Advanced Secondary Schools – FV, FVI (GDY Publications Company Ltd DSM

Tranter C.J (2006) " Advanced Level Mathematics 4th edition, Hroder Murray, London NW 1 3BH

Advanced Mathematics for Advanced Secondary Schools by Tellem Majigwa

**8. GENERAL STUDIES**

J,K (1974) Ujamaa – Essays onsoualism, London Oxford University Pries

Saluhaya M.C (2003) Advanced Level General Studies

Nyambari N (2018) Advanced Level GS notes form 5 and 6 Nyambari Nyangwine Publishers DSM

Mkapa B.W (2019), My life, My purpose: Mkuki na Nyota Publishers, DSM

**9. KISWAHILI**

(i) ***KISWAHILI 1***

1. Nadharia ya lugha ya Kiswahili: Kidato cha Tano na Sita – Nyambari Nyangine na Masebo (2010)
2. Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu (SAMAKISA): Sekondari na Vyuo – Kihore, Y.M. na Masamba, D.P.B: TUKI (2003)
3. Kamusi ya Kiswahili Sanifu, Toleo la pili: English – Swahili Dictionary – TUKI
4. Sarufi miundo ya Kiswahili ( SAMIKISA) – Masamba, D.P.B.

(ii) ***FASIHI .***

Kamusi ya Kiswahili Sanifu

1. Nadharia ya Fasihi kidato cha Tano na Sita – Masebo - +Oxford University Press
2. Tahakiki Vitabu Teule Vya Fasihi Kidato cha 5 na 6 – Nyambari Nyangine na Masebo

**TAMTHILIA (WALAU VITABU VIWILI)**

1. Kivuli kinaish – Said Ahmed Mohamed – Oxford University Press
2. Kwenye Ukingo wa Thimu – Ibrahim Hussein – Oxford University Press
3. Nguzo Mama – Penina Muhando (1982)
4. Morani – Emanuel Mbogo (1993)

**RIWAYA (WALAU VITABU VIWILI)**

1. Vuta ni kuvut, 4th ed. – Mbunda Msokile (2009)
2. Kufikirika, 4th ed. – Shaban Robert – Mkuki na Nyota
3. Mfadhili – Hussein Tuwa (2007) – Macmillan Aidan
4. Usiku utakapokwisha, 2nd ed. – Mbunda Msokile (2007) – Macmillan Aidan

USHAIRI (WALAU VITABU VIWILI)

1. Kimbunga: Toleo la Tatu (3rd ed. – Haji Gora Haji (1995) – TUKI
2. Chungu Tamu – Theobald Mvungi
3. Mapenzi Bora – Shaban Robert – Mkuki na Nyota publishers
4. Fungate ya Uhuru – Mohamed S. Khatibu – Macmillan Aidan